



Mchango wa Muziki wa Bongo Flewa katika Kuibua Msamiati Mpya na Maana Mpya za Kiswahili nchini Tanzania

Ernest Daimon Haonga

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam, Tanzania

Uwasilishaji wa Makala

Kupokelewa: 2025-05-16
Kurekebishwa: 2025-11-14
Kukubaliwa: 2025-11-20
Kuchapishwa: 2025-11-23

Maneno Muhimu

Bongo Flewa
Ethnopragsmatiki
Msamiati
Muziki

Jinsi ya Kurejelea Makala:

Haonga, E. D. (2025). Mchango wa Muziki wa Bongo Flewa katika Kuibua Msamiati Mpya na Maana Mpya za Kiswahili nchini Tanzania. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 3(2), 89-98.

Copyright © 2025



Ikisiri

Makala hii inachunguza jinsi muziki wa Bongo Flewa unavyochangia katika kuibua msamiati mpya na kutoa maana mpya katika lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Kwa kutumia Nadharia ya Uchanganuzi wa Maana katika Mukdadha wa Jamii (Ethnopragsmatiki), makala inachambua jinsi lugha inavyotumika katika mazingira halisi ya kijamii na kitamaduni. Makala hii ilitumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui, ambapo nyimbo kumi (10) za Bongo Flewa zilichaguliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa ili kubaini mabadiliko ya msamiati na maana. Data zilipatikana kutoka kwenye tovuti zinazohifadhi nyimbo "lyrics" kama vile "Genius.com" na "LyricFind". Matokeo yanaonesha kuwa muziki wa Bongo Flewa unachangia kwa kiasi kikubwa katika kuibua maneno mapya na kubadilisha maana ya maneno yaliyokuwepo. Hii ni kwa kuwa Wasanii wanatumia lugha ya taswira, mafumbo, na msamiati wa kisasa kuakisi masuala ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi. Pia, uchunguzi unaonesha kuwa Bongo Flewa si tu burudani, bali chombo cha kuboresha na kuendeleza Kiswahili, huku ukichangia katika ukuaji wa msamiati na uhamasishaji wa matumizi ya lugha katika jamii. Hivyo, wataalamu wa lugha na jamii hawana budi kutambua na kuthamini mchango huu muhimu katika ukuaji wa Kiswahili kama lugha hai na inayobadilika.

Utangulizi

Lugha ni chombo hai kinachokua, kubadilika, na kuakisi mabadiliko yanayotokea katika jamii husika. Kama ambavyo jamii hubadilika kijamii, kiutamaduni, kiuchumi, na kiteknolojia, vivyo hivyo lugha nayo hubadilika na kukua kulingana na muktadha wa mabadiliko hayo. Katika muktadha wa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania, muziki umeibuka kama nyanja muhimu za kijamii zinazochochea mabadiliko ya lugha, hususan katika uundaji wa msamiati mpya na utoaji wa maana mpya kwa baadhi ya maneno yaliyopo. Sanaa hii, imekuwa jukwaa muhimu linalorahisisha kuenea kwa istilahi mpya, ufufuo wa maneno ya kale, na kubadilika kwa maana za maneno, hali ambayo inachochea katika ukuaji na utajiri wa Kiswahili kama lugha hai ya mawasiliano.

Nchini Tanzania, historia ya muziki wa Kiswahili inarudi nyuma hadi enzi za muziki wa Taarab, muziki wa dansi, na nyimbo za harusi, ambazo zimekuwa si tu burudani, bali pia vyanzo vya kuendeleza lugha Muziki ni Sanaa ya kupangilia au kuunganisha sauti kwa mpangilio maalumu ili kuleta uhuru wa kujieleza, burudani, hisia, au ujumbe. Utafiti wa Ojode (2017) umebainisha kuwa nyimbo za Taarab zimechangia kwa kiasi kikubwa katika kuibua msamiati mpya unaokidhi mazingira ya kisasa, huku zikibeba sitiari, methali, na maneno yenye maana fiche yanayohusiana na masuala ya kijamii na maisha. Jambo hili linajitokeza pia katika muziki wa Bongo Flewa, ambapo



wasanii hutumia msamiati na mitindo ya lugha inayoakisi maisha yao ya sasa, mitazamo yao kuhusu jamii, pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo katika mazingira ya kisasa. Kwa mujibu wa Lupogo (2024), Thiong'o na Barasa (2019), Bongo Fleva ni aina ya muziki unaotumia lugha ya kisasa, mwongozo wa biti "beat" za kigeni, na kuisitiza masuala ya kijamii na ya kisiasa. Muziki huu umeibuka kama nyenzo muhimu ya kisanaa na kijamii inayochangia katika ukuaji na ubunifu wa matumizi ya maneno katika lugha.

Hivyo basi, utafiti huu unalenga kuchambua kwa kina jinsi muziki wa Bongo Fleva unavyokuza msamiati mpya na kutoa maana mpya katika Kiswahili, kwa kutumia Nadharia ya Ethnopragsmatiki, kuelewa muktadha wa kijamii na kitamaduni wa matumizi ya maneno husika katika Kiswahili. Kwa msingi huo, makala hii itachunguza mchango wa muziki wa Bongo Fleva katika kuibua msamiati mpya na maana mpya katika Kiswahili nchini Tanzania. Lengo kuu ni kubaini na kuchambua maneno na misemo mipya inayotokana na nyimbo za Bongo Fleva, na kujadili jinsi matumizi ya lugha katika muziki yanavyoakisi na kuathiri mabadiliko ya lugha kijamii na kiutamaduni.

Kiunzi cha Nadharia na Methodolojia ya Utafiti

Sehemu hii inatoa maelezo ya kina kuhusu nadharia iliyotumika na mbinu zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Maelezo haya yanasaidia kuweka msingi wa kitaaluma wa kuelewa namna muziki wa Bongo Fleva unavyochangia katika uendelezaji wa msamiati na uibuaji wa maana mpya za maneno katika lugha ya Kiswahili.

Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi wa Maana katika Muktadha wa Jamii (Ethnopragsmatiki). Nadharia hii, iliyoasisiwa na Wierzbicka (1991) na kupanuliwa na Goddard (2006), inajikita katika kuelewa maana ya maneno na misemo katika lugha kwa kuzingatia mazingira maalum ya kitamaduni na kijamii ambayo lugha hutumiwa. Goddard (2006) anaeleza kuwa, Nadharia ya Ethnopragsmatiki inasisitiza kuwa, maana ya maneno haeleweki vyema isipokuwa ikichambuliwa kupitia lensi ya desturi, maadili, imani, na mtazamo wa jamii husika. Tofauti na nadharia za kiisimu za kijadi zinazojikita kwenye sarufi au muundo wa maneno, Ethnopragsmatiki huzingatia maana ya maneno katika mazingira ya matumizi halisi, ambapo misemo na maneno hubeba uzito wa kijamii na kisemantiki unaotofautiana kati ya jamii moja na nyingine.

Nadharia hii ilichaguliwa kwa sababu ya umuhimu wake wa kipekee katika kuchambua lugha ya muziki wa Bongo Fleva. Muziki huu ni taswira halisi ya mazungumzo ya mtaani na huakisi maisha, mitazamo, na tamaduni za vijana wa Tanzania. Kwa hiyo, kuweka mchanganuo wake ndani ya mfumo wa Ethnopragsmatiki kunasaidia kuelewa siyo tu maneno yanamaanisha *nini*, bali pia *kwa nini* na *jinsi gani* maana hizo zimekuwa na zinavyoathiri na kuakisi muktadha wa kijamii wa Tanzania. Nadharia ya Ethnopragsmatiki inasaidia kuchambua na kuelewa maana ya maneno kulingana na muktadha wa jamii yanamotumika.

Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchambuzi wa maudhui. Mbinu hii inafaa zaidi kwa sababu inakuwezesha kubainisha na kuchambua mifumo ya lugha na maana katika nyimbo, na kuyaelezea katika muktadha wa kijamii (Krippendorff, 2013). Kulingana na kanuni za uchambuzi wa maudhui wa kina, nyimbo kumi (10) za Bongo Fleva zilichaguliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Nyimbo hizo ni *Sitaki Demu* wa Juma Nature (2003); *Mchepuko* wa Rayvanny (ft. Phina) (2023); *Mikasi* wa Albert Mangwea (ft. Mox, Mkoloni na Rah P) (2003); *Mbona* wa PNC (ft. Mr. Blue)



(2015); *Zali la Mentali* wa Professor Jay (2003); *Kila Mtu na Demu Wake* wa Mr. Nice (2000); *Demu Wangu* wa Mr. Two Joseph Mbilinyi ft Mr Paul (2000); *Maokoto* wa Billnass Ft. Marioo (2023), *Usichoke* wa Mwasiti (2025); na *Sizonje* wa Mrisho Mpoti (2016). Uchaguzi huu ulifanywa kwa kuzingatia vigezo kadhaa muhimu, ikiwemo uhalisia wa lugha ya mtaani, matumizi ya msamiati mpya, pamoja na kuwapo kwa matumizi ya maneno yenye maana fulani ya msingi kuibua maana mpya. Aidha, sampuli ilihusisha nyimbo zinazowakilisha mada mbalimbali kama vile mahusiano, uchumi na siasa, ili kuhakikisha mtazamo mpana wa utafiti. Vilevile, kigezo cha umaarufu kilizingatiwa katika kuchagua nyimbo zilizosikilizwa zaidi na zenye athari kubwa katika jamii.

Data za kimaudhui zilikusanywa kwa kutazama video za nyimbo husika kwenye majukwaa rasmi ya “*YouTube*” ili kuthibitisha hati za maneno (lyrics) na kuchunguza muktadha wa kiutamaduni uliooneshwa kupitia picha. Hati za maneno zilipatikana kutoka kwenye tovuti zinazohifadhi “lyrics” kama vile “*Genius.com*” na “*LyricFind*”. Baada ya kukusanywa, maneno na misemo mahususi yalitambuliwa na kuchambuliwa kwa kuzingatia vigezo vitatu: kwanza, maana ya msingi ya neno endapo ipo; pili, maana mpya inayojitokeza katika muktadha wa wimbo; na tatu, mchango wa muktadha wa kijamii, kisiasa au kiuchumi katika kutoa maana hiyo mpya.

Ili kuongeza uhalali na kuaminika kwa matokeo, data zilizokusanywa zilijadiliwa na wataalamu wawili (2) wa lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Tanzania. Wataalamu hawa waliteuliwa kutokana na utaalumu wao katika nyanja za isimu na utamaduni wa Kiswahili. Wataalamu walipitia uchambuzi wa awali wa data na kutoa maoni kuhusu uhalali wa muktadha wa kijamii uliotolewa kwa maneno yaliyochambuliwa. Maoni haya yalisaidia kuboresha ufasili wa matokeo. Data lengwa iliyotokana na mchakato huu ilikuwa ya maoni ya kitaalamu (na ilikubaliwa kupitia mchakato wa uthibitishaji. Kwa njia hii, mbinu ya uchambuzi wa maudhui na usampulishaji lengwa ziliwezesha ufahamu wa kina wa jinsi Bongo Flewa inavyokuza msamiati na maana mpya katika Kiswahili.

Matokeo ya Utafiti

Uchambuzi wa maudhui ya nyimbo za Muziki wa Bongo Flewa umeonesha kuwa muziki huu umechangia kwa kiwango kikubwa katika kuibua msamiati mpya na kuyapatia maneno yaliyokuwapo maana mpya kama inavyoelezwa sehemu ifuatayo:

Msamiati Unaohusu Mahusiano ya Kimapenzi

Muziki wa Bongo Flewa umekuwa na mchango katika kuzalisha na kuendeleza msamiati unaohusiana na mapenzi, hisia, na mahusiano ya kijinsia. Maneno haya, ingawa mara nyingi huzaliwa katika muktadha wa burudani na ubunifu wa kisanaa, hujikita katika mawasiliano ya kila siku na hatimaye kuunda mitindo mipya ya usemi katika Kiswahili. Utafiti huu unabainisha kuwa neno *demu* lenye maana ya nguo ya zamani inayofungwa na wanawake kichwani au kiunoni wakati wa kufanya kazi ngumu, limepata maana mpya ya *mpenzi wa kike* au *mwanamke kijana* aliye katika uhusiano wa kimapenzi kupitia nyimbo za bongo flewa. Matumizi ya neno *demu* katika maana hii mpya yameenea kiasi cha kuonekana kama sehemu ya lugha ya kawaida ya vijana. MATHALANI, katika wimbo wa *Sitaki Demu* (2003), msanii Juma Nature (Kiroboto) anaghani:

*Walimwengu walikwisha niambia kuwa demu wangu mimi hafai,
Mimi nikawabishia nikaona wao ndio hawafai,
Hivi sasa mi najuta sitaki demu silitaji demu.*



Matumizi ya neno *demu* katika ubeti huu yanabeba dhana ya *mpenzi wa kike*, lakini kwa mtindo usio rasmi unaotokana na muktadha wa lugha ya vijana. Maneno ni vyombo vya kisanaa na vya kijamii vinavyoakisi mitazamo, maadili, na ubunifu wa jamii. Katika nyimbo za bongo fleva, neno “*demu*” linatumika kumaanisha “*mpenzi wa kike*” au “*mwanamke aliyeko katika uhusiano wa kimapenzi*,” na mara nyingi hutolewa katika muktadha wa mitindo ya vijana.

Vivyo hivyo, katika nyimbo kama *Kila Mtu na Demu Wake (Mr. Nice, 2007)* na *Demu Wangu (Mr Two Joseph Mbilinyi ft Mr Paul 2000)*, neno *demu* linachukua maana ya *mpenzi wa kike* aliyepangwa katika muktadha wa hisia, mvuto, na uhusiano wa kijamii. Kwa kutumia Nadharia ya Ethnopragsmatiki ya Goddard (2006), maana ya neno *demu* haiwezi kufungika tu katika kamusi, bali inategemea muktadha wa kijamii na kitamaduni wa jamii inayotumia lugha hiyo. Nadharia hii inaonesha kuwa lugha ni kioo cha mazoea na mitazamo ya kijamii: maneno hubadilika maana kulingana na namna jamii inavyoyatumia na kusawiri dhana. Hivyo, neno *demu* ni kielelezo cha ubunifu wa lugha katika muziki, kinachoashiria mitindo ya kijamii na kijinsia. Matumizi yake yanaonesha jinsi sanaa inavyobeba na kusambaza dhana za kijinsia, huku pia ikichangia mabadiliko na upanuzi wa msamiati wa Kiswahili katika muktadha wa kisasa.

Vilevile, neno *mchepuko* limepata umaarufu kupitia mashairi ya muziki wa kizazi kipya, likimaanisha *mwenza wa pembeni nje ya ndoa au uhusiano rasmi*. Neno hili limebadilisha namna jamii inavyozungumzia mahusiano ya kificho kwa kutumia msamiati usio wa moja kwa moja lakini wenye kueleweka kwa urahisi Neno hilo kabla ya kupata maana mpya katika muziki wa Bongo fleva lilikuwa na maana ya njia ya mkato au njia ya kupita pembeni ili kuepuka foleni. Katika wimbo wa Mchepuko (Rayvanny Ft. Phina_2023), neno *mchepuko* linatumika kama ifuatavyo:

“Unapoelekea *mchepuko* wangu,
Unanichosha *mwenzenu*,
Mchepuko we *mchepuko* we
Mchepuko niachie baby wangu”

Matumizi ya neno “*mchepuko*” katika wimbo wa Rayvanny Ft. Phina yanaonesha jinsi msamiati unavyobadilika kulingana na muktadha wa kijamii na kitamaduni. Kulingana na Nadharia ya Ethnopragsmatiki, maana ya maneno hubainika kupitia muktadha wa mawasiliano, lengo la msemaji, na dhana ya kijamii inayozunguka matumizi ya lugha. Kwa hivyo, neno *mchepuko* linapotumika katika nyimbo hizi, linachukua maana inayorejelea uhusiano wa kificho na mpenzi wa pembeni, likionesha mitazamo ya kijamii kuhusu mahusiano yasiyo rasmi na tabia za kijinsia. Hali hii inaonesha wazi jinsi msamiati unaohusiana na mahusiano unavyobadilika na kuibua maana mpya kulingana na muktadha wa kijamii na kitamaduni. Kwa ujumla, neno *mchepuko* linapotajwa katika nyimbo hizi, linabeba tafsiri zinazotokana na muktadha wa kipragsmatiki wa mawasiliano, hali za kijamii, na mitazamo ya kitamaduni ya jamii inayotumia lugha hiyo.

Vilevile, msamiati mwingine mpya ulioibuka kupitia muziki wa Bongo Fleva ni neno *milupo*. Katika wimbo wa Mikasi (2007) wa Albert Mangwea, neno *milupo* linatumika kumaanisha wanawake wanaojiuza kimapenzi. Katika muktadha wa wimbo huu, neno *milupo* linatumiwa kumaanisha wanawake wanaoshiriki katika biashara ya ngono, na linatumiwa katika mashairi kama vile:

“*Milupo* tutapata wapi?
Milupo labda mitaa ya kati,
So, tunaenda vipi kwa miguu au kwa basi?...”



Matumizi ya neno *milupo* (wingi wa neno mlupo) katika wimbo huu yanaonesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyopokea msamiati kulingana na muktadha wa kijamii na kitamaduni wa jamii inayotumia lugha hiyo. Katika utafiti wa Spemba (2014), wimbo huu unatajwa kama mfano wa nyimbo zinazohamasisha tabia hatarishi kama vile uasherati, matumizi ya pombe, na dawa za kulevywa. Hata hivyo, utafiti huu unajenga hoja kwa kuegemea kwenye Nadharia ya Ethnopragsmatiki ya Goddard (2006) kwamba maana ya maneno hubainika siyo kwa tafsiri ya kamusi pekee, bali pia kupitia muktadha wa kijamii na kitamaduni wa watumiaji wake. Kwa hiyo, msanii anakwepa kutumia neno gumu kama "malaya" ambalo linaweza kuwa na ukakasi kijamii. Hii ni mbinu ya pragmatiki inayokubalika kijamii, ambapo msanii anapenda kutoa ujumbe unaoeleweka na wasikilizaji wa mtaani bila kuvunja vigezo vya heshima au hatari ya kudhalilisha moja kwa moja. Kwa hivyo, neno *milupo* linatoa suluhisho la pragmatiki: linatoa maana ya kimaadili na kijamii inayofahamika, linashikilia hisia za jamii za mtaani, na kwa wakati mmoja linapunguza ukali wa maneno kama *malaya*. Hii inathibitisha kwamba matumizi ya neno "*milupo*" ni mfano halisi wa jinsi msamiati wa Kiswahili cha mtaani inavyoundwa na kuamuliwa na mitazamo ya kijamii na kitamaduni, huku ukitumia mbinu za pragmatiki kudhibiti athari za kijamii za maneno makali.

Msamiati Unaohusu Fedha na Uchumi

Uchambuzi wa nyimbo hizi unadhihirisha kuwa lugha ni zao la muktadha wa kijamii, kama inavyopendekezwa na Nadharia ya Ethnopragsmatiki ya Goddard (2006), ambapo maana ya maneno hutegemea muktadha wa kijamii na kitamaduni wa watumiaji wake. Mathalani, neno *mapene* katika nyimbo za Kiswahili za bongo fleva linatumiwa kumaanisha fedha zinazohitajika katika mahusiano ya kijamii na limeenea miongoni mwa wanajamii kupitia nyimbo za Bongo Fleva. Kwa maneno mengine, *mapene* si tu alama ya rasilimali za kifedha, bali ni ishara ya matarajio ya kijamii na kiutamaduni yanayohusiana na uwapo wa mchango wa kifedha katika mahusiano ya kila siku. Uchambuzi wa wimbo wa *Mbona* (2006) wa PNC ft. Mr. Blue unaonesha matumizi ya neno hili katika mistari ifuatayo:

*"Jawabu bado sijapata kabisa,
Kipi nilichofanya mpaka ukanitosa,
Au kwa sababu mapene sijashika x 2"*

Katika ubeti huo, msanii anamlalamikia mpenzi wake kwa kumtosa au kumkataa, akieleza kwamba kutopewa *mapene* (fedha) ndiyo sababu ya kutopewa ushirikiano. Kielelezo hiki cha lugha kinadhihirisha kwamba msamiati wa Kiswahili ni zana ya kufikisha maana kulingana na muktadha wa kijamii. Katika muktadha huu, neno *mapene* linabeba maana ya fedha au rasilimali, likihusishwa na matarajio ya kijamii katika mahusiano, na linaweza kutofautiana kulingana na muktadha wa nyimbo na jumuiya ya wasikilizaji. Matumizi haya ya neno *mapene* yanaonesha jinsi wasanii wa Bongo Fleva wanavyotumia pragmatiki ya lugha kuakisi mitazamo ya kijamii na mahitaji ya kiuchumi ya mtaani, huku wakitumia maneno yenye maana ya dhana zinazojulikana na jamii yao. Uchambuzi wa pragmatiki unaonesha kuwa msamiati unachukua maana na thamani kutoka katika mitazamo ya kijamii ya jamii inayotumia lugha, likiweka kumbukumbu ya maadili, heshima, na usawa wa kijamii.

Vilevile, uchambuzi wa nyimbo ulibaini matumizi ya neno *ngawila* katika wimbo wa *Zali la Mentali* (2004) wa Professor Jay, na neno *maokoto* katika wimbo wa *Maokoto* (Billnass Ft. Marioo 2023) kumaanisha fedha. Matumizi ya maneno haya yanaakisi mitindo ya kijamii na mitazamo ya kijinsia ya mtaani, ambapo lugha inatumika kama chombo cha kufikisha ujumbe wa kijamii bila kutumia maneno makali au ya dhahiri. Nadharia ya Ethnopragsmatiki inaonesha wazi kwamba lugha ni zao



la muktadha wa kijamii: maneno kama ankara, mkwanja, mapene, ngawila, na maokoto yanabeba maana inayotegemea uhusiano wa kijamii, mitazamo ya kijinsia, na mbinu za kifasihi zinazoweza wasanii kufikisha ujumbe kwa usahihi na usiozidi. Hii inaonesha jinsi nyimbo za Bongo Flewa zinavyoweza kuibua msamiati mpya, kuipa maneno yaliyopo maana mpya, na kuonesha uhusiano wa karibu kati ya lugha, jamii, na utamaduni wa mtaani. Katika jamii ya Waswahili, neno “fedha” au “pesa” ndilo lingetarajiwa kutumika, lakini wasanii wanachagua maneno mbadala ili kuwasilisha msisitizo wa kisemantiki unaoendana na mitazamo, mitindo ya maisha na mawasiliano ya vijana wa sasa.

Uchambuzi katika utafiti huu unaonesha kuwa maneno mengine mapya huibuka katika nyimbo za Bongo Flewa yanapozungumzia hali ya kiuchumi ya maisha ya watu katika jamii. Maneno haya huibua mifumo ya kijamii inayotofautiana kulingana na kipato, ikiwemo ile inayowarejelea watu wenye kipato cha juu na wenye kipato cha chini. Moja ya neno linalorejelea mtu mwenye kipato kikubwa na cheo kikubwa ni *pedeshee* katika wimbo wa *Usichoke* (2025) wa Mwasiti. Katika wimbo huo msanii anasema: *Wewe ndiye pedeshee wangu, nguzo ya mafanikio yangu*. Neno *pedeshee* ni mwangwi wa neno ‘*pedejee*’ linalotumiwa sana katika muziki wa dansi Tanzania, ambapo wanamuziki walikuwa wakiimba majina ya “mapedejee” waliokuwa wakifadhili burudani au kuonesha ukarimu wao kwa fedha. Baada ya hapo, neno hili liliendelea kupanuka na kuhamia kwenye Bongo Flewa, likibeba maana hiyo hiyo ya mtu mwenye fedha nyingi, anayeishi kifahari, na mara nyingi anayehusiana na majina makubwa katika muziki na burudani.

Kwa jumla, neno pe-de-je (PDG) lililoibuka katika muziki wa Kikongo na kubadilika kuwa *pedejee* na *pedeshee* katika Kiswahili cha mtaani, limebeba maana ya mtu mwenye hadhi ya kifedha na kijamii anayejulikana kwa ukarimu na udhamini wake kwa wanamuziki. Katika muktadha wa vijana wa Bongo Flewa, matumizi ya neno hili hayalengi tu utajiri, bali pia hadhi, heshima na nafasi ya kijamii anayopata tajiri huyo kupitia muziki na burudani. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ethnogramatiki, maana ya *pedejee* haiwezi kuelezeka nje ya muktadha wa kijamii na kitamaduni unaotumika; ni muktadha huo unaoipa nguvu ya kisemantiki na kufanya iwe alama ya maisha ya kifahari, ukarimu na mtindo wa maisha unaoenziwa na vijana katika muziki wa kisasa.

Msamiati wa Burudani na Mitindo ya Vijana

Utafiti unabainisha kwamba muziki wa Bongo Flewa umejidhihirisha kama chombo muhimu cha ubunifu wa kisemantiki na kisanii katika lugha ya Kiswahili. Kupitia nyimbo za wasanii mbalimbali, msamiati mpya umeibuka, huku maneno mengine ya Kiswahili yaliyokuwepo awali yakipewa maana mpya kulingana na muktadha wa kijamii, burudani na utambulisho wa vijana. Muziki huu unatumia mchanganyiko wa Kiswahili cha mitaani, Kiingereza, na hata maneno kutoka lugha nyingine, hali ambayo inachochea kuzaliwa kwa maneno mapya yanayopenya kwenye mawasiliano kila siku. Hali hii huufanya muziki kuwa njia ya uhalalishaji wa lugha isiyo rasmi kuingia katika Kiswahili cha kawaida. Kwa msingi wa Nadharia ya Ethnogramatiki, muktadha wa nyimbo hizi unathibitisha kwamba maana ya neno haitokani na kamusi tu, bali na namna linavyotumika katika matukio ya mawasiliano na burudani. Mfano unaoibua dhana hii ni wimbo wa Mikasi (2007) wa Albert Mangwea (Maarufu kama Mangwea Ft. ft Mox, Mkoloni na Rah P). Katika kibwagizo cha wimbo huu, wasanii wanasema:

*“Mitungi, blanti, mikasi,
Kama ukitaka kuvinjari nasi,
Basi mfukoni mwako uwe safi”*



Hapa, maneno *mitungi*, *blanti*, na *mikasi* yametumiwa kurejelea pombe, dawa za kulevya, na uasherati mtawalia. Maneno haya yametumika tofauti kabisa na ya maana zake za kimsingi (mitungi - vyombo vya kuhifadhia maji; mikasi - vifaa vya kunyolea) na kupewa tafsiri mpya zinazojengwa katika muktadha wa starehe, matumizi ya pombe, kuvuta bange/dawa za kulevya, na kufanya ngono na wanawake wanaojiuza. Huu ni udhihirisho wa mbinu ya upanuzi wa maana ambapo maneno ya Kiswahili ya kawaida hupewa maana mpya ili kuendana na mazingira ya kijamii ya burudani. Kwa hiyo, makala hii inajenga hoja kuwa muziki wa Bongo Flewa si burudani pekee, bali ni chombo kinachoshiriki kikamilifu katika mchakato wa uundaji wa msamiati mpya na upanuzi wa maana, hali inayoendeleza ukuaji na uhai wa Kiswahili katika kizazi cha sasa.

Sambamba na hayo, utafiti huu unabainisha kwamba Muziki wa Bongo Flewa hauibui maneno mapya pekee, bali pia hupanua maana ya maneno yaliyokuwepo awali katika Kiswahili. Kwa mfano, maneno kama *kujirusha* na *kujiachia*, ambayo kihistoria yalitumiwa kuelezea vitendo vya kimsingi au matendo ya kila siku, yamepewa maana mpya katika Bongo Flewa. Katika muziki huu, neno *kujirusha* linamaanisha kushiriki kikamilifu katika starehe au sherehe, mara nyingi likihusiana na kutumia pesa au kufurahia maisha bila hofu, wakati *kujiachia* linatofautiana na maana ya kiasili ya kupumzika au kujitenga; sasa linahusiana na furaha kamili, kujieleza kwa uhuru, na kushiriki kikamilifu katika burudani bila kuwa na kizuizi chochote. Mfano huu unaweza kuonekana katika wimbo wa *Mikasi* (2007) na *Kila Mtu na Demu Wake* (2007) wa Mangwea, na Mr. Nice mtawalia. Katika nyimbo hizo, maneno haya hutumika kuunda taswira za mvuto wa maisha ya vijana mijini na heshima ya kijamii inayotokana na uwezo wa kifedha na mtindo wa maisha.

Msamiati Unaohusu Masuala ya Kisiaa

Kwa muktadha huu, wimbo kama *Sizonje* wa *Mrisho Mpoto* (2016) na nyimbo mbalimbali za *Roma Mkatoliki* kama *Zimbabwe* (2017), zimekuwa uwanja wa kukuza Kiswahili kwa kutumia sitiari, taswira ya majina ya wanasiasa, na kupanua maana ya maneno ya kawaida ili kutoa maana mpya zinazohusiana na hali halisi ya muktadha halisi wa Kisiaa Tanzania. Katika wimbo *Sizonje*, Mrisho Mpoto anatumia majina ya wanasiasa na misemo ya kila siku ili kujenga maudhui ya kisasa. Mfano muhimu ni pale ambapo anatumia dhana ya “*Sizonje*” na “*nyumba yetu*”. Katika muktadha wa wimbo, *Sizonje* anachukuliwa kama mgeni au mtu wa nje anayejipenyeza ndani ya jamii kulinda rasilimali za jamii. Kama Nadharia ya Ethnopragsmatiki ya Goddard (2006) inavyoelekeza kuhusu kupata maana ya neno kupitia muktadha halisi, maana ya neno *Sizonje* inapatikana kupitia muktadha wa jamii na wakati unaolipa neno hilo uzito wa kiuhalisia. Hapa, *Sizonje* anawakilisha Rais John Magufuli ambaye amekabidhiwa nyumba yenye milango wazi. Katika kibwagizo cha wimbo huu, msanii anasema:

*“Sizonje hii ndio nyumba yetu... Milango ipo wanapita
madirishani... Ingia uyaone, maajabu ya nyumba
yetu...”*

Vilevile, taswira ya “*nyumba*” inatumika kama sitiari ya taifa la Tanzania. Msanii anaeleza kwamba wakati Rais Magufuli anaingia madarakani, alikuta “*nyumba iko wazi*”, akimaanisha kuwa nchi ilikuwa katika hali dhaifu ya kiuchumi na kijamii, hivyo kulikuwa na hatari ya kuachia wageni kuinyonya. Isitoshe, msanii anatumia taswira ya *milango* akimaanisha taratibu na kanuni zilizowekwa kuisimamia nyumba (nchi), na taswira ya *madirisha* kama njia ambazo siyo sahihi kuruhusu wageni kuingia nchini. Kwa hiyo, nyimbo kama *Sizonje*, zinathibitisha hoja kuu ya Goddard (2006) kwamba maana za maneno hupatikana na kueleweka kupitia muktadha wa kitamaduni na kijamii wa watumiaji wa lugha. Kupitia sitiari, taswira, na majina ya kijiografia au



wanasiasa, wasanii hawa wanapanua msamiati wa Kiswahili na kuufanya uwe chombo cha kuwasilisha maudhui ya kisasa kuhusu uzalendo, ulinzi wa rasilimali, changamoto za kisiasa na kijamii, pamoja na wajibu wa viongozi kwa wananchi wao.

Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Makala hii inaonesha namna maneno ya kawaida yanavyopata maana mpya katika nyimbo za Bongo Flewa, hasa pale ambapo wasanii wanatumia lugha ya taswira na mafumbo kuelezea masuala ya kijamii na kisiasa. Katika wimbo wa Nandy “*Kunjani*” (2019), kwa mfano, neno *kufolo* linatumiwa kuashiria kufuata maelekezo au maagizo, ikionesha utii au ushirikiano katika muktadha wa kijamii na kisiasa (Mgalula, 2020). Hali hii inapanua maana ya maneno ya Kiswahili ya kawaida, ikitengeneza maana mpya inayoweza msanii kueleza hoja kwa njia isiyo ya moja kwa moja, huku akivutia hadhira na kusambaza ujumbe wa kijamii.

Utafiti unajitofautisha na tafiti zilizotangulia kama zile za Ali (2014), Mugaya (2022), na Masatu (2023), ambazo zilijikita zaidi katika uchambuzi wa msamiati mpya katika nyimbo za Bongo Flewa bila kuangazia kwa kina jinsi maneno yanavyopanuliwa kimaana kupitia taswira na mafumbo (Yesaya, 2020). Hapa, mizizi ya maana mpya inaonekana wazi, kama vile katika wimbo wa Mangwea wa *mikasi* (2003), ambapo neno *mikasi* linapokea maana ya nguvu au juhudi zinazohitajika kufanikisha jambo fulani. Katika nyimbo za Mr. Nice “*Fagilia Wote*” (2002) na Professor Jay “*Ndio Mzee*” (2001), ambapo maneno yanayohusiana na hadhi ya jamii kama *mastaa* yanatumika kuonesha heshima, utambulisho, na mafanikio ya kifedha yanayopambanua na watumiaji wa lugha.

Kwa mujibu wa Mugaya (2022), nyimbo ni sehemu muhimu ya ujifunzaji na maendeleo ya lugha ya Kiswahili, hasa kwa watoto na vijana, hali inayothibitisha kuwa mchango wa sanaa katika kuendeleza msamiati hauishii kwenye burudani pekee, bali pia una nafasi katika elimu isiyo rasmi. Muziki wa Bongo Flewa unachangia kwa kiasi kikubwa katika uundaji wa msamiati mpya katika Kiswahili. Wasanii hutumia lugha ya taswira, mafumbo, na maneno yanayohusiana na mitindo ya mitandao kuwasilisha masuala ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi (Englert, 2024). Kwa mfano, katika wimbo wa Hussein Machozi “*Addicted*” (2011) na wimbo wa Mwasiti “*Nalioua Pendo*” (2008), neno *vibes* linatumiwa kuelezea hali ya furaha au starehe inayotokana na muziki, huku likiibua pia maana ya ziada inayohusiana na mitindo ya kijamii na hali ya kimahaba (Mto & Msoffe, 2021). Njia hii ya kimaandishi inathibitisha kuwa muziki wa Bongo Flewa ni chombo chenye nguvu cha kuunda, kueneza, na kueneza maana mpya katika maneno ya lugha.

Muktadha wa kijamii na kisiasa una nafasi muhimu katika uundaji wa maana mpya. Kwa mfano, msanii Nandy hupenda kutumia taswira na mafumbo kuelezea maelekezo au tabia zinazohitajika kufuata katika jamii, na hivyo kutoa nafasi ya kueleza hoja za kijamii na kisiasa kwa njia ya kifasihi (Mugo, Mwithi, & Mayaka, 2022). Hii inaonesha dhana ya Pragmatiki, kwamba maana ya neno hutegemea sana muktadha wa kijamii na kitamaduni, na siyo ufafanuzi wa kamusi pekee (Ogechi, 2022). Kwa hivyo, maneno kama *kufolo* au *vibes* yanakuwa na maana ya ziada inayotegemea muktadha wa nyimbo na hoja inayokusudiwa kuwasilishwa.

Matokeo haya yanaonesha kuwa utafiti unachangia katika kuelewa namna lugha ya Kiswahili inavyokua na kupanuka kupitia burudani ya muziki, ikitofautisha na tafiti zilizotangulia kwa kushughulikia kwa kina mbinu za taswira, mafumbo, na muktadha wa kijamii na kisiasa (Kasiga, 2023a) na Chebet-Choge (2020). Hii inathibitisha upekee wa utafiti huu, kwani ulilenga si tu kuorodhesha msamiati mpya, bali pia kuelewa muktadha wa maana na mbinu za kisanaa zinazotumika katika kuunda maana hiyo (Nyandwaro & Malugu, 2024).



Hitimisho

Makala hii imejikita katika uchambuzi wa nyimbo za Bongo Fleva, ukichunguza kwa kina namna wasanii wa muziki huo wanavyotumia lugha ya Kiswahili kuibua msamiati mpya, kuhuisha maneno ya kale, na kutoa maana mbadala kwa maneno yaliyokuwepo. Bongo Fleva, kama mtindo wa muziki unaoakisi maisha ya watu, umejipambanua kuwa jukwaa hai la ubunifu wa lugha, ambapo wasanii hujenga misamiati inayobeba hisia, mitazamo na changamoto za kijamii kwa kutumia Kiswahili cha kisasa kinachovutia hadhira pana. Kimsingi, Bongo Fleva si tu burudani, bali ni chombo cha mawasiliano kinachochochea mabadiliko ya lugha kwa kasi kikubwa na kwa upana wake. Msamiati unaoibuliwa kupitia nyimbo hizi mara nyingi huakisi muhtadha wa maisha ya kila siku – kuanzia mahusiano ya kimapeenzi, hali ya uchumi, siasa za mitaani, hadi mitindo ya mavazi na teknolojia. Kwa mfano, maneno kama “mademu,” “mchizi,” “milupo,” pedeshee” ni mifano ya misamiati inayojitokeza katika nyimbo na baadaye kuingia katika matumizi ya kawaida katika jamii. Hii inaonesha dhana ya Pragmatiki, kwamba maana ya neno hutegemea sana muhtadha wa kijamii na kitamaduni, na siyo ufafanuzi wa kamusi pekee. Matokeo ya utafiti yanachangia katika kuelewa namna lugha ya Kiswahili inavyokua na kupanuka kupitia burudani ya muziki.

Marejeo

- Ali, A. (2014). *Matumizi ya Lugha katika Tamthilia za Kiswahili*. Dar es Salaam University Press.
- Billnass (Ft. Marioo). (2023). *Maokoto* (Song). On *Bongo Hits 2023*. Bongo Records.
- Chebet-Choge, S. (2020). Kiswahili katika Utawala na Siasa Tanzania. *Jenga Journal*, 8(2), 112-125.
- Englert, B. (2024). *Language Choice and Youth Identity in Bongo Fleva: Networks and Norms* (Master's Thesis, University of Dar es Salaam).
- Goddard, C. (2006). *Ethnopragmatics: Understanding Discourse in Cultural Context*. Mouton de Gruyter.
- Goddard, C., & Wierzbicka, A. (2004). Cultural Scripts: What are They and What are They good for? *Intercultural Pragmatics*, 1(2), 153–166. <https://doi.org/10.1515/iprg.2004.1.2.153>
- Juma Nature. (2003). *Sitaki Demu* (Song). On *Mtaa Mentality*. Nature Records.
- Krippendorff, K. (2013). *Content Analysis: An Introduction to its Methodology* (3rd ed.). SAGE Publications.
- Lupogo, I. (2024). Utohoaji na Matumizi ya Maneno Changamani katika Lugha ya Kiswahili: Mifano ya Mkanganyiko wa Maana na Matumizi ya Neno “Bongofleva” Nchini Tanzania. *Jarida la Dira ya Lugha*, 1(1), 25-40. <https://jadilu.seku.ac.ke/index.php/jadilu/article/view/26>.
- Masatu, F. (2023). *Kuchunguza Maendeleo ya Ubunifu katika Tamthilia ya Kiswahili* (Tasnifu ya Uzamivu). The Open University of Tanzania.
- Masuala Mtambuko katika Mtaala wa Umilisi. *Jarida la Mwangwa wa Lugha*, 9(1), 117-128.
- Mgalula, S. (2020). *Dhima ya Taswira katika Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya: Mifano kutoka kwa Nasibu Abdul na Mrisho Mpoto* (Master's Thesis). University of Dodoma.
- Mr. Nice. (2007). *Kila Mtu na Demu Wake* (Wimbo). On *Mtaa Classic*. Nice Music.
- Mrisho Mpoto. (2016). *Sizonje* (Wimbo). On *Nyimbo za Ukweli*. Mpoto Records.
- Mto, G. R., & Msoffe, M. J. (2021). Language Trend in Contemporary Tanzanian Music: Assessing the Impact of English Usage in Bongo Fleva Lyrics. *Business Education Journal*, 2(1), 13-25.
- Mugaya, T. S. (2022). Nafasi ya Nyimbo katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili kwa Watoto wa Elimu ya Awali. *Mulika Journal*, 41(2), 242-262.
- Mugo, L. W., Mwithi, F., & Mayaka, G. (2022). Mikakati ya Usemi Inayodhihirisha Uanaharakati wa Kijamii katika Muziki wa Genge nchini Kenya. *Eastern Africa Journal of Kiswahili (EAJK)*, 1(1), 6-15.
- Mwasiti. (2025). *Usichoke* (Wimbo). On *Forever Hits*. Mwasiti Music.
- Nandy. (2019). *Kunjani* (Wimbo). On *The African Princess*. Nandy Music.



-
- Nyandwaro, L. K., & Malugu, A. (2024). Nafasi ya Nyimbo za Kizazi Kipya katika Kufundishia Ojode, J. O. (2017). *Uchanganuzi Kipragmatiki wa Sitiari katika Nyimbo za Taarab: Mfano wa Mzee Yusuf na Mwanahawa Ally, Unguja* (Tasnifu ya Uzamivu). Kisii University.
- Ogechi, N. (2022). Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Maendeleo ya Afrika Mashariki. *Chama Cha Kiswahili Afrika Mashariki*, 1(1), 1-20.
- PNC (Ft. Mr. Blue). (2015). *Mbona* (Wimbo). On *Street Power*. PNC Records.
- Professor Jay. (2003). *Zali la Mentali* (Wimbo). On *Machazo*. Jay Music.
- Rayvanny (Ft. Phina). (2023). *Mchepuko* (Wimbo). On *Flowers*. WCB Wasafi.
- Roma Mkatoliki. (2017). *Zimbabwe* (Wimbo). On *Mkatoliki Volume 2*. Roma Records.
- Spemba, A. (2014). Athari za Nyimbo za Kizazi Kipya kwa Vijana wa Miji: Uchunguzi wa Wimbo wa Mikasi. *Mulika Journal*, 41(2), 242-262.
- Thiong'o, J., & Barasa, D., (2019). Intonation as Metaphors in the song "Kama Nikifa Kesho" by Diamond Platnumz. *Alternation: Interdisciplinary Journal for the study of Arts and the Humanities in Southern Africa, Special Edition*, 25: 341-356.
- Wierzbicka, A. (1991). *Cross-cultural Pragmatics: The Semantics of Human Interaction*. Mouton de Gruyter.
- Yesaya, S. (2020). Ufemerali katika Nyimbo za Muziki wa Bongoflewa nchini Tanzania: Mifano kutoka Nyimbo Teule. *Jarida la Mwanga wa Lugha*, 5(1), 1-18.